



EDI LIMITED
PO BOX 393, BUKOBA
KAGERA, TANZANIA



TANGAZO

MWALIKO WA KUOMBA KUANDIKISHWA KAMA MZABUNI WA KUKODISHA MAGARI KWA KAMPUNI YA EDI LIMITED

Utangulizi

EDI Limited (Namba ya Usajili 43600) ni kampuni yenye Makao Makuu Bukoba –Tanzania lakini inayotambulika kimataifa katika kuendesha shughuli za kiutafiti na inaongoza tangu ilipoundwa mwaka 2002, EDI Ltd imezidi kukua na kuwa moja ya kampuni za Kitafiti zinazoheshimika katika Afrika Mashariki na imekuwa inashika nafasi ya juu kama taasisi binafsi ya kiutafiti barani Afrika.

EDI Ltd inaheshimika sana ndani ya Tanzania na Afrika kutokana na kazi zake za kiuchunguzi na ukusanyaji wa data zenye ubora wa hali ya juu na ina uzoefu wa zaidi ya miaka 12 ya kusimamia miradi mikubwa ya ukusanyaji wa data pamoja na tathmini za matokeo katika - sampuli mbalimbali za watu.

EDI Ltd inaendesha tafiti kote Tanzania na mara nyingi hulazimika kusafiri umbali mrefu katika maeneo yanayofikika kwa kutumia magari ya “4 wheels” tu. Timu za watafiti huweza kuwa kati ya watu 5 na 70. Magari huweza kukodishwa kwa vipindi vya kati ya wiki moja hadi wiki sita au zaidi.

Mwaliko

EDI Ltd inawakaribisha watu binafsi au kampuni **kujiandikisha** nasi EDI Ltd kama mmoja wa wanaopenda kutoa huduma hiyo ya Kukodisha Magari tunayohitaji. Watoa huduma hii ya kukodisha magari wanaweza kujiandikisha kutoka Mkoa wowote hapa Tanzania lakini wanatakiwa kuzingatia masharti ya Uandikishaji yaliyopo hapa chini.

Masharti ya Kujiandikisha

Ili uweze kustahili kujiandikisha lazima utimize masharti yafuatayo:

1. Mkodisha Magari lazima awe mzoefu na mwenye kuaminika na kuweza kutupatia magari yanayohitajika kama atafanikiwa kwenye mchakato wa zabuni.
2. Magari yote lazima yawe na uwezo wa kutumika bila shida. Magari yote yatakayoletwa wakati wa mchakato wa zabuni yatakaguliwa kwa makini na pia kutathminiwa wakati wa kupokelewa.
3. Wazabuni lazima wawe na uwezo wa kubadilisha gari lolote litakaloharibika wakati wa kazi bila kuchelewesha kazi za EDI Ltd.
4. Wazabuni watatakiwa kulipa gharama za uendeshaji wa gari hadi mwisho wa kipindi cha kukodishwa. Katika mazingira maalumu, EDI Ltd itakuwa tayari kulipa kiasi cha fedha kama muda wa kukodishwa gari ni zaidi ya majuma manne (4)
5. EDI Ltd inahitaji wazabuni wenye magari yafuatayo:
 - i. Magari ya 4 x 4 – yenye uwezo wa kubeba watu wanne (4) au zaidi.
 - ii. Mabasi madogo – yenye uwezo wa kubeba abiria 12 na zaidi. Aina ya 4x4 inapende;ewa zaidi
6. Wazabuni watatakiwa kuthibitisha idadi ya magari na aina zilizotajwa hapo juu pamoja na idadi ya abiria.
7. Wazabuni lazima waorodheshe Mkoa ambako EDI Ltd inaweza kukodi na kutumia magari yao.
8. Wazabuni lazima wathibitishie kama wao ni kampuni iliyosajiliwa au kama ni watu binafsi. Kama ni Kampuni, basi mzabuni atulettee nakala ya Cheti cha Usajili wa Kampuni (*Business Registration Certificate*). Mzabuni lazima atupatie nakala ya TIN.



EDI LIMITED
PO BOX 393, BUKOBA
KAGERA, TANZANIA



TANGAZO

9. Wazabuni lazima watupatie orodha ya majina ya Maofisa na njia za mawasiliano (simu ya mkononi au barua pepe) ya watu wawili ambao wamewahi kutumia huduma yako kwa kukodi magari katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Njia ya Kujisajili

Wale wanaopenda kujiorodhesha nasi watahitajika kujaza Fomu yetu ya Usajili pamoja na viambatanisho na kuziwasilisha EDI Ltd kama ifuatavyo.

Fomu yetu ya Usajili inaweza kupatikana kwa njia zifuatazo:

1. Tuma Barua pepe kwa Katibu Kamati ya Zabuni ya EDI Ltd anwani: **procurement@edi-africa.com** ukiomba nakala ya Fomu.
2. Kwa kuzipata kimtandao kwa tovuti: www.edi-global.com/procurement
3. Kwa kupiga simu (**+255 783 135 299**) ofisi za EDI Limited, Kibeta, Kituo kipya cha biashara Rugambwa, Kwenye makutano ya barabara Kanazi na ile iendayo KEMPS , Bukoba na kuja kuzichukua kwa mkono.

Kitakachotokea baada ya Kujisajili

Kama umetimiza masharti yote ya usajili, taarifa zako zitahifadhiwa kwenye Orodha ya wasafirishaji wa EDI LTD “*EDI Ltd Preferred Vehicle Supplier List*”. Katika kipindi kisichozidi miezi 12 EDI Ltd itafanya mapitio na kutangaza waliochaguliwa kutoa huduma hii kwa ajili ya miradi mbalimbali wanayotekeleza.

Kwa kulingana na mahitaji ya mikoa itakayo tembelewa na aina ya magari yanayohitajika, Wazabuni walioko katika orodha kuu watakaribishwa kuwasilisha kwenye bahasha iliyofungwa kuomba kutoa huduma ya kukodisha magari yanayohitajika. Zabuni hizo zitafanyiwa uchambuzi kulingana na vigezo vya mahitaji ambavyo vilitolewa wakati wa kuleta zabuni.

Mahali pa kuwasilisha zabuni:

Taarifa za Usajili zipelekwe kwa barua pepe kwa: **procurement@edi-africa.com**. Wazabuni wanaweza pia kutuma kwa:

Katibu, Kamati ya Manunuzi EDI Ltd
S L P 393
Bukoba
Kagera
Tanzania

TAFADHALI ZINGATIA:

Tafadhali hakikisha kuwa unatuma kumbukumbu ZOTE zilizohitajika pamoja na Fomu ya Usajili wa zabuni ya magari.

**MUDA WA KUFUNGWA KWA USAJILI NI SAA 10 Jumatatu TAREHE
30Novemba, 2015**